SOUTH CAROLINA DEPARTMENT OF PUBLIC HEALTH

# Walaka wa Taratibu za Faragha

**Walaka huu unaelezea jinsi taarifa za matibabu kukuhusu wewe zinaweza kutumiwa na kuwekwa wazi na jinsi unaweza kuzipata taarifa hizi. *Tafadhali pitia kwa uangalifu.***

## Ahadi yetu Kuhusiana na Taarifa zako za Afya:

Idara ya Afya ya Umma ya South Carolina (South Carolina Department of Public Health - DPH) inajitolea kulinda faragha ya taarifa zako za afya. Tunatengeneza kumbukumbu ya huduma ya afya na huduma zingine unazopokea ili kukupatia huduma bora na kufuata matakwa ya sheria.

Walaka huu unaelezea jinsi tunavyoweza kutumia au kachilia taarifa zako za afya, wajibu wetu kuhusiana na utumiaji wa uachiliaji wa taarifa zako za afya, na haki zako kuhusiana na taarifa zako za afya. Tunahitajika na sheria kuhakikisha kwamba taarifa za afya ambazo zinakutambulisha wewe zinakuwa za binafsi, kukupa Walaka huu wa majukumu yetu ya kisheria na taratibu za faragha kuhusiana na taarifa zako za afya, kufuata masharti ya Walaka wetu wa sasa, na kukujulisha iwapo itatokea kuvujifu wa taarifa zako za afya ambazo hazijahifadhiwa kwa usalama.

Walaka huu unatumika kwa kumbukumbu zote za huduma zako zilizotengenezwa na DPH, iwe zimetengenezwa na mfanyakazi wa kliniki au mtoa huduma za afya. Taratibu zinazoelezewa kwenye Walaka huu zitafuatwa na kliniki zote za DPH, mjumbe wowote wa kundi la watu wanaojitolea tunaowaruhusu kukusaidia wakati unapokuwa kwenye jingo hili, na waajiriwa wote, wafanyakazi na watumishi wengine wa DPH.

Iwapo una maswali kuhusu Walaka huu wa Taratibu za Faragha, tafadhali wasiliana na:

**DPH Privacy Officer**
South Carolina Department of Public Health
P.O. Box 2046, West Columbia, SC 29171
(803) 898-3318 or compliance@dph.sc.gov

## Jinsi DPH Inavyotumia na Kuachilia Taarifa za Afya

Vipengele vifuatavyo vinaelezea njia ambazo DPH hutumia na kuachilia taarifa za afya.

- **Kwa Matibabu.** Tunatumia taarifa kukupatia matibabu au huduma. Tunaweza kuachilia taarifa zako za afya kwa wahudumu kama vile madaktari, wauguzi, wataalamu, wanafunzi wa uuguzi, au watumishi wengine wa DPH ambao wanakuhudumia. Tunaweza pia kuachilia taarifa kwa watu wa nje ya DPH ambao wanasaidia katika kutoa huduma kama vile wanafamilia au watoa huduma za afya wengine. Kwa mfano, daktari anayekutibu kwa ajili ya jeraha anaweza kuhitaji kujua kuhusu sukari yako kwa madhumuni ya matibabu. Vitengo au idara tofauti za DPH zinaweza kushirikisha taarifa kukuhusu wewe ili kuratibu mahitaji tofauti tofauti, kama vile utoaji dawa, kazi za maabara au rufaa.
- **Kwa ajili ya Malipo.** Tunaweza kutumia na kuachilia taarifa zako za afya kukuandikia Ankara na kukusanya malipo kwa ajili ya matibabu yako na huduma kutoka kwenye kampuni ya bima au mtu wa tatu, au kupata uthibitisho wa kabla kwa ajili ya matibabu kutoka kwenye mpango wako wa afya. Kwa mfano, tunatoa taarifa za afya kukuhusu wewe kwa mpango wako wa bima ya afya ili walipie huduma zako.
- **Kwa ajili ya Shughuli za Huduma za Afya.** Tunaweza kutumia na kuachilia taarifa zako za afya kwa ajili ya shughuli za huduma za afya muhimu katika kuendesha kliniki na kuhakikisha kwamba wagonjwa wetu wote wanapokea huduma bora. Kwa mfano, tunaweza kuchanganya taarifa za afya kuhusu wagonjwa wengi wa kliniki ili kuamua huduma gani za ziada tunapaswa kutoa, huduma gani hazihitajiki, na iwapo tiba mpya zinafanya kazi vizuri. Tunaweza kuweka wazi taarifa kwa madaktari, wauguzi, wataalamu, wanafunzi wa uuguzi, na watumishi wengine wa kliniki kwa ajili ya kupitia na kujifunza. Tunaweza kuondoa taarifa ambazo zinakutambulisha wewe kutoka kwenye taarifa hizi za kitabibu ili wengine waweze kutumia kujifunza huduma za afya na utoaji wa huduma za afya bila kujifunza wewe ni nani.
- **Utafiti.** Katika hali Fulani, tunaweza kutumia na kuachilia taarifa za afya kwa ajili ya madhumuni ya utafiti. Kwa mfano, mradi wa utafiti unaweza kulinganisha afnya na uponaji wa wagonjwa ambao wametumia dawa moja na wale wengine ambao wametumia dawa nyingine kwa hali sawa. Miradi yote ya utafiti lazima kwanza iidhinishwe kupitia hatua maalumu za tathmini ili kuweka mlingano wa mahitaji ya utafiti na hitaji lako kwa ajili ya faragha.
- **Kama inavyohitajika na Sheria.** Tutaachilia taarifa zako za afya inapohitajika kufanya hivyo na sheria za shirikisho au sheria za nchi.
- **Kuzuia Hatari Kali kwa Afya au Usalama.** Tunaweza kutumia na kuachilia taarifa zako za afya inapohitajika kuzuia hatari kubwa kwa afya au usalama wako au afya na usalama wa mtu mwingine au umma.

## Matumizi na Kuachilia Taarifa zako Katika Hali Maalumu

- **Uchangiaji wa viungo na Tishu.** Kama wewe ni mchangiaji wa viungo, tunaweza kuachilia taarifa zako za afya kama inavyohitajika kwa mashirika ambayo yanashughulikia ununuaji wa viungo, macho au upandikizaji wa tishu au kwenye benki ya viungo.
- **Shughuli Maalumu ya Serikali.** Tunaweza kuachilia taarifa zako za afya kwaajili ya madhumuni maalumu ya serikali, ikiwemo shughuli za kijeshi na wazee, usalama wa taifa na shughuli za kiintelijensia, huduma za kinga za Rais na wengine, ubainishaji wa tiba sahihi kwaajili ya Idara za Maofisa wa Serikali, taasisi za kurekebisha tabia na watekelezaji wa sheria katika hali za vizuizi, au kwa ajili wa mafao ya umma.
- **Fidia ya Wafanyakazi.** Tunaweza kuachilia taarifa za afya kukuhusu wewe kwa ajili ya fidia ya wafanyakazi au mipango inayolingana nayo ambayo inatoa mafao kwa ajili ya majeruhi au ugonjwa unaohusiana na kazi.
- **Shughuli za Afya ya Umma.** Tunaweza kuachilia taarifa zako za afya kwa ajili ya shughuli za afya ya umma ili kuzuia au kudhibiti ugonjwa, majeruhi au ulemavu; kutoa taarifa matukio muhimu kama vile vizazi na vifo; kutoa taarifa za chanjo kwa msajili wa serikali; kutoa taarifa za udhalilishaji au utelekezaji wa mtoto; kutoa taarifa za matokeo a matibabu au matatizo ya bidhaa; kuwajulisha watu juu ya kukumbuka bidhaa; kumjulisha mtu ambaye anaweza kuambukizwa ugonjwa au anaweza kuwa katika hatari ya kupata au kusambaza ugonjwa au hali; kuwajulisha mamlaka husika ya serikali juu ya tuhuma za udhalilishaji, utelekezaji au ukatili majumbani kama inavyohitajika au kukubalika kisheria.
- **Shughuli za usimamizi wa Afya.** Tunaweza kuachilia taarifa zako za afya kwa Wakala wa Usimaizi wa Afya kwa ajili ya shughuli zilizokubaliwa kisheria kama vile ukaguzi wa mahesabu, uchunguzi, ukaguzi, na au utoaji leseni.
- **Mashtaka na Migogoro.** Tunaweza kuachilia taarifa zako za afya kwa amri ya mahakama au utawala au kujibu maombi ya uvumbuzi, au taratibu zingine za kisheria.
- **Utekelezaji wa Sheria.** Tunaweza kuachilia taarifa za afya yako kwa maofisa wa utekelezaji wa sheria:
  - Katika kujibu amri ya Mahakama, hati ya kuitwa mahakamani, kuitwa mahakamani au taratibu zinazolingana na hizo;
  - Kumbainisha au kumpata mtuhumiwa, mkimbizi, ushahidi wa vitu, au mtu aliyepotea;
  - Kama wewe ni mhanga wa kosa la uvunjifu wa sheria,na makubaliano yako au katika hali Fulani, kama tunashindwa kupata makubaliano yako;
  - Kuhusu kifo tunaamini kinaweza kuwa kimesababishwa na tukio la uvunjifu wa sheria;
  - Kitendo cha kijinai katika kliniki au idara ya afya; na
  - Katika hali ya dharura kutoa taarifa za uvunjifu wa sheria; mahali pa tukio au wahanga; au kitambulisho, maelezo au mahali pa mtu ambaye amefanya kosa.
- **Maofisa Wachunguzi wa Vifo, Wachunguzi wa Dawa na Waongozaji wa Mazishi.** Tunaweza kuachilia taarifa za afya kwa ofisa uchunguzi wa kifo au mchunguzi wa dawa, kwa mfano kubainisha marehemu au kutambua sababu ya kifo, au waongozaji wa mazishi kama inavyohitajika kutekeleza majukumu yao.
- **Wakazi.** Kama wewe ni mkazi wa kwenye taasisi za kurekebisha tabia kama vile jela au uko chini ya ulinzi wa maofisa watekelezaji wa sheria, tunaweza kuachilia taarifa za afya kukuhusu wewe kwa taasisi hiyo au maofisa watekelezaji wa sheria iwapo uachiliaji ni muhimu kwa ajili ya taasisi kukupatia huduma ya afya, kulinda afya yako na usalama wa wengine, au kwa ajili ya usalama na ulinzi wa taasisi ya kurekebisha tabia.
- Tunaweza kuweka taarifa zako za afya katika mfumo wa kielekroniki na kushirikisha watoa huduma za afya wengine kupitia ubadilishanaji wa taarifa za afya, isipokuwa uombe kwamba tusifanye hivyo.
- Hatutatumia au kuachilia taarifa zako za afya kwa madhumuni ya kutangaza au shughuli za kuchangisha fedha. Hatutatumia au kuweka wazi maelezo ya matibabu ya kisaikolojia bila idhini yako ya maandishi (yenye mataraji finyu ya matibabu Fulani, malipo au huduma za afya). Hatutauza taarifa zako za afya.
- Chini ya Sheria ya South Carolina, lazima tusiachilie kukumbuku za matibabu yako bila idhini yako ya kimaandishi, ila kama ilivyoelekezwa vinginevyo na sheria. Lazima kufuate masharti mengine ya ziada kwa aina Fulani za taarifa, ikiwemo taarifa inayohusiana na magonjwa ya kuambukizwa kwa njia ya ngono, VVU, TB, magonjwa mengine ya kuambikiza, mpango wa uzazi, WIC, udhibiti wa madawa, matumizi ya vitu vya kulevya,na afya ya akili.

  **Hatutaachilia taarifa za STD/VVU isipokuwa**:

  - Kwa madhumuni ya takwimu katika namna kwamba hakuna mtu mmoja moja anayeweza kutambulika;

- Kwa makubaliano ya watu wote waliobainishwa kwenye taarifa iliyoachiliwa;
- Katika kiwango ambacho ni muhimu kutekeleza sheria za nchi na taratibu kuhusiana na udhibiti na matibabu wa magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya ngono (STD);
- Kwa tatibu katika hali ambayo ni muhimu ili kulinda afya au maisha ya mtu yeyote;
- Katika hali zinazohusisha watoto, jina la motto na taarifa za matibabu kumuhusu motto lazima ziripotiwe kwa mawakala sahihi iwapo taarifa ya udhalilishaji au utelekezaji inahitajiwa na sheria; au
- Iwapo motto ana UKIMWI au ameambukizwa Virusi Vya UKIMWI (VVU), na anahudhuria shule ya umma katika shule ya awali hadi darasa la tano, tutamjulisha mkuu wa wilaya ya shule na muuguzi au wataalamu wengine wa afya waliopangiwa kwenye shule ambayo mtoto anahudhuria.

## Haki za Taarifa zako za Afya

Una haki zifuatazo kuhusiana na taarifa za afya ambazo DPH inazo kukuhusu wewe:

- **Haki ya Kukagua au Kupata Nakala ya Taarifa zako za Afya.** Unaweza kuomba nakala ya taarifa za afya ikiwemo, dawa, Ankara au taarifa za malipo ya huduma za afya kutoka kwenye idara ya afya. Haki hizi zinajumuisha kupata nakala ya taarifa za vipimo moja kwa moja kutoka kwenye maabara. Kwa maombi, tutakupatia jina la maabara.

  Ili kufikia taarifa zako za afya, ikiwemo taarifa zozote za vipimo zilizoratibiwa na Taasisi ya Maabara ya DPH, lazima uwasilishe maombi kwa maandishi. Idara ya Afya ya DPH ya ndani au Taasisi ya Maabara zinaweza kukupa Idhini ya Kuachilia Taarifa za afya, iwapo utaomba. Katika hali Fulani, unaweza kuombwa kutoa kithibitisho cha utambulisho ili kupata taarifa zako za afya.

  Iwapo tunahifadhi taarifa zako za afya katika kumbukumbu za kielekroniki, na unaomba nakala ya kielektroniki, tutakupatia taarifa hizo katika mfumo wa kielektroniki na mfumo ambao wewe unaomba kama inaweza kuzalishwa. Kama haiwezi, tutakupa taarifa katika mfumo wa kielektroniki unaosomeka kama tutakavyokubaliana sisi na wewe. Kama utatuelekeza kufanya hivyo, tutasafirisha taarifa zako moja kwa moja kwa mtu au shirika unalotaka zipelekwe. Tunaweza kukudai gharama kidogo kwa ajili ya kutoa nakala, kusafirisha, na usambazaji unaohusiana na maombi yako, ikiwemo gharama za kifaa cha kielektroniki kinachobebeka iwapo utaomba taarifa zako katika mfumo huo. Tutajibu mambo yako yote halali kwa ajili ya taarifa zako za afya ndani ya siku thelathini au kukujulisha kushindwa kwetu kufanya hivyo.

  Katika kesi chache, tunaweza kukataa ombi lako. Iwapo ombi lako litakataliwa, unaweza kuomba kupitia tena kukataliwa kwako.
- **Haki ya Kurekebisha.** Iwapo unaamini taarifa zako za afya si sahihi au hazijakamilika, unaweza kutuomba kurekebisha taarifa kwa kutuma maombi kimaandishi kwa Ofisa Faragha ukielezea sababu ya kuamini taarifa zako zinapaswa kurekebishwa. Tunaweza kukataa ombi lako iwapo utaomba kurekebisha taarifa ambazo zilitengenezwa na sisi; siyo sehemu ya taarifa za afya zinazohifadhiwa na au kwa ajili ya DPH; si sehemu ya taarifa ambazo ungeruhusiwa kukagua na kutoa nakala; au taarifa zako za afya ni sahihi na zimekamilika. Una haki ya kuomba marekebisho ili maradi DPH inahifadhi taarifa hizo.
- **Haki Kupata Idadi ya Ruhusa.** Una haki ya kuomba orodha ya ruhusa za taarifa zako za afya tulizotoa. Hii haitajumuisha taarifa za afya zilizotolewa ili kukupa matibabu, kupata malipo ya huduma, au kwa ajili ya madhumuni ya kiutawala au utendaji (isipokuwa imeachiliwa kupitia kumbukumbu za afya za kielektroniki tulizotengeneza za taarifa zako katika miaka mitatu kabla ya ombo lako); Ruhusa kwaajili ya dhumuni la kiusalama; ruhusa kwenye sehemu za kurekebisha tabia au watekelezaji wengine wa sheria; ruhusa zilizoidhinishwa na wewe; ruhusa kwa watu waliohusika na huduma yako ya afya; na ruhusa zilizofanywa zaidi ya miaka sita kabla ya ombi lako.
- Lazima uwasilishe ombi lako katika maandishi kwa Ofisa Faragha, ikieleza kipindi cha muda ambao hauwezi kurudi nyuma zaidi ya miaka sita. Ombi lako linapaswa kuonyesha unataka orodha hiyo katika mfumo gani (kwa mfano, kwa karatasi au kielektroniki). Orodha ya kwanza unayoomba ndani ya kipindi cha miaka 12 itakuwa bila malipo. Tunaweza kukudai gharama kwa ajili ya kukupatia orodha za ziada. Kama hivyo ndivyo, tutakujulisha kuhusu gharama na unaweza kuondoa au kuboresha ombi lako kabla ya kudaiwa gharama.
- **Haki ya Kuomba Vizuizi.** Una haki ya kuomba zuio juu ya taarifa za afya tunazotumia au kuweka wazi kuhusu wewe kwa ajili ya matibabu, malipo au shughuli za huduma ya afya. Unapaswa kuwa na haki ya kuomba ukomo juu ya taarifa za afya tunazozitoa kukuhusu kwa mtu mwingine ambaye anahusika na huduma yako au malipo ya huduma yako kama vile mwanafamilia au rafiki. Kwa mfano, unaweza kuomba kwamba tusitumie au kuweka wazi taarifa kuhusu chanjo au huduma Fulani uliyopata. Unaweza kuomba kwamba hatushirikiki taarifa zako kupitia ubadilishanaji wa wa taarifa za afya kwa njia ya kielektroniki.
- Hatuhitajiki kukubali ombi lako isipokuwa uwe umelipia kipengele cha huduma ya afya "kutoka nfukoni" na unaomba taarifa zisiwasilishwe kwa mpango wako wa afya kwa ajili ya malipo au madhumuni ya shughuli za husuma za afya. Kama tukikubali, tutafuata ombi lako isipokuwa taarifa zinahitajika ili kukupatia matibabu ya dharura.
- Kuomba vizuizi, lazima ufanye maombi yako kwa maandishi kwa Ofisa Faragha. Katika ombi lako, lazima utuambie: (1) taarifa unazotaka kuweka ukomo; (2) iwapo unataka kuzuia utumiaji wetu, uwekaji wazi au vyote; na (3) kwa nani unataka vizuizi vitumike, Kwa mfano, kuweka wazi kwa mwenza wako.
- **Haki ya Kuomba mawasiliano ya Siri.** Una haki ya kuomba kwamba tuwasiliane nawe kwa siri kuhusiana na masuala yako ya afya katika namna Fulani au katika eneo fulani. Kwa mfano, unaweza kuomba kwamba tunawasiliana nawe kwa kazini tu au kwa njia ya barua. Kuomba mawasiliano ya siri, lazima ufanye ombi lako kimaandishi kwa Ofisa Faragha. Hatutakuuliza sababu ya ombi lako. Tutashughulikia maombi yote muhimu. Ombi lako lazima libainishe ni kwa namna gani au wapi unapenda tuwasiliane nawe.
- **Haki ya Kuchagua Mwakilishi.** Una haki ya kumpa mtu mwingine mamlaka ya kufanya maamuzi kuhusu taarifa zako za afya, kama vile nguvu ya mamlaka ya uwakilishi. Kama mtu ni mlezi kisheria, mtu huyo anaweza pia kuwa na haki na kufanya chaguzi kuhusu taarifa zako za afya.
- **Haki Kupata Nakala ya Karatasi Ya Walaka Huu.**Una haki ya kuomba nakala ya karatasi ya walaka huu wakati wowote kwa kuwasiliana na Ofisa Faragha aliyetajwa kwenye Walaka Huu. Unaweza kupata nakala ya walaka huu kwenye tovuti yetu: **dph.sc.gov**

## Mabadiliko ya Walaka Huu

Tuna haki ya kubadili walaka huu. Tunaweza kufanya walaka ulioboreshwa au kubadilishwa kutumika kwaajili ya taarifa za matibabu ambazo tayari tunazo kukuhusu vile vile taarifa zozote tutakazopokea mbeleni. Tutabandika nakala ya walaka wa sasa kwenye kliniki ya DPH na majengo mengine. Walaka utajumuisha katika ukurasa wa kwanza, sehemu ya chini upande wa kulia kwenye kona, tarehe ya kuanza kufanya kazi. Kwa kuongezea, kila wakati unapopata matibabu au huduma za afya katika kliniki yoyote ya DPH, tutakupa nakala ya walaka wa sasa unaotumika.

## Malalamiko

Iwapo unaamini haki yako ya faragha imekiukwa, unaweza kufungua malalamiko na Ofisa Faragha wa DPH au Idara ya Afya na Ofisi ya Huduma za Binadamu yaa Haki za Raia. Kufungua malalamiko na DPH, wasilisha malalamiko yako kimaandishi kwa Ofisa Faragha katika anuani iliyoorodheshwa kwenye Walaka Huu. Kufungua malalamiko na Ofisi ya haki za Raia, wasilisha malalamiko yako kimaandishi kwa:

**Centralized Case Management Operations**
U.S. Department of Health and Human Services
200 Independence Avenue, S.W.
Room 509F HHH Bldg
Washington, DC 20201
Customer Response Center: 1-800-368-1019
Fax: (202) 619-3818 • TDD: 1-800-537-7697
Email: OCRComplaint@hhs.gov

Hautaadhibiwa au kuwekewa kisasi dhidi yako kwa kufungua malalamiko.

## Matumizi mengine ya Taarifa za Afya

Walaka huu unaelezea na kutoa mifano ya njia zilizoruhusiwa taarifa zako za afya zinaweza kutumiwa au kuachiliwa. Tutakuomba kwa ajili ya ruhusa ya maandishi kabla ya kutumia au kuachilia taarifa zako za afya wa ajili ya madhumuni ambayo hayajajumuishwa kwenye Walaka huu au inavyohitajika na sheria. Ukitupatia ruhusa ya maandishi kutumia au kuachilia taarifa, unaweza kubadilisha mawazo yako na kuondoa ruhusa yako wakati wowote kwa kumjulisha Ofisa Faragha kimaandishi. Iwapo utaondoa ruhusa yako, hatutatumia au kuachilia taarifa kwa dhumuni hilo. Hata hivyo, hatutaweza kurudhisha idhini yoyote iliyotolewa kwa ruhusa yako, na tunahitajika kuzuia kumbukumbu zetu za huduma ambayo tulikupatia.